

# Maadili ya Sayansi ya Neva (Neuroethics) Mabango na Hotuba

Jumuiya ya Kimataifa ya Maadili ya Sayansi ya Neva ((International of Neuroethics Society (INS)) inawaalika watafiti na madaktari kutuma mikhtasari ya maonyesho yatakayohusishwa katika mkutano wa kila mwaka wa INS mnamo tarehe 2 hadi 4 Novemba, 2022. Mkutano huu ni wa mseto na utajumuisha fursa za kushiriki mtandaoni na pia ana kwa ana huko Montreal, Kanada.

## MAELEZO YA KUTUMA MUKHTASARI

Mikhtasari zitaelezea kuhusu utafiti au usomi unaohusiana na taaluma ya maadili ya sayansi ya neva (neuroethics) ambao ungependa kuwasilisha. Wakati wa kutuma mukhtasari, ambatanisha maelezo ya aina ya maonyesho unayopendekeza yazingatie: maonyesho ya bango (kwa mfano la kibinafsi au ana kwa ana), hotuba mafupi (dakika 5) au hotuba marefu (dakika 12).

Mikhtasari itasaidia kuunga ratiba ya kongamano na mikhtasari bora zaidi itangaziwa kwenye jarida litakaloharirirwa kutokana na mkutano wa mwaka huu.

## MADA YA KONGAMANO

Mada ya mkutano huu ni **'Kuhuisha maadili ya sayansi ya neva katika uuguzi, utafiti na sheria'**.

Idadi ya vikao vitapangiliwa kushughulikia mada hii na vitazingatia maudhui ya kinga, uchunguzi wa magonjwa, tiba mpya, teknolojia na utafiti, urejeshi wa afya ya neva na mwisho wa maisha.

Nia kuu ya INS ni kuwezesha kutangamana kwa taaluma tofauti tofauti, mijadala ya kimataifa, na kujumuika kwa kiwango kikubwa zaidi wanaougua hali za neva na watetezi wao katika kongamano hili. Ratiba ya vikao itatangazwa baada ya miezi chache, pindi wawakilishi wa vikao watakapo chaguliwa na kukubali wito.

2022 INS MKUTANO  
WA KILA MWAKA

## AINA ZA MAONYESHO

- › Bango (mtandaoni au ana kwa ana)
- › Hotuba fupi (dakika tano)
- › Hotuba ndefu (dakika kumi na mbili)

## MAAGIZO YA KUWASILISHA MIKHTASARI

Mikhtasari ziwe na urefu wa maneno 250-350, na ziandikwe kwa kiingereza. Kila mukhtasari uwe na sehemu hizi:

- › Kichwa
- › Waandishi
- › Mashirika husika ya maandishi
- › Marejeleo na mafichuzi
- › Mapendekezo ya vifaa vya kuwasiliisha onyesho
- › Mapendekezo ya lugha

## UWANACHAMA KATIKA INS

Uwanachama katika INS sio miongoni mwa masharti ya kuwasilisha mukhtasari. Lakini, mwandishi mmoja, kati ya kundi la maandishi wa mukhtasari, anapaswa kuuonyesha utafiti katika kongamano naye sharti awe mwanachama wa INS wakati wa maonyesho.

## KUWASILISHA MIKHTASARI

Tarehe ya mwisho ya kupokelewa kwa mikhtasari ni **Mai 31**, (saa 11:30pm, wakati wa mashariki). Mikhtasari iliyochelewa ama isiyo kamili haitakubaliwa.

[NEUROETHICSSOCIETY.ORG/CALL](https://neuroethicsociety.org/call)



Jumuiya ya Kimataifa ya maadili ya sayansi na neva ni muungano wa kitaaluma wa wanasayansi, wasomi, wauguzi na wanasheria walio na malengo na maoni ambatani ya kiadili au kisheria au ya kijamii yanayohusika na maendeleo ya sayansi ya neva. Wanachama wa jumuiya hii wanajihusisha na taaluma maridhawa na wana zana hitajika za kuwasilisha jumbe kuhusu umuhimu na athari za ujuzi, utaalumu, na matumizi kwa afya ya wanadamu yanayoibuka kutokana na sayansi ya neva.